

bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na tani 4,839 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia tisa.

Kuongezeka kwa mgao wa fedha kwa Wakala wa Barabara

Wakala wa Barabara zinazopokea fedha toka Mfuko wa Barabara ni mme ambao ni Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, TANROADS, na TARURA. Katika kipindi cha miaka mitatu Bodi, iligawa jumla ya shilingi trilioni 2.124 kwa wakala husika.

Mgao wa Fedha za Mfuko wa Barabara kwenda TANROADS uliongezeka kutoka shilingi milioni 351,464 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi miiioni 489,305 mwaka 2017/18. Jumla ya shilingi trilioni 1.327 zilipelekwa TANROADS katika kipindi cha miaka mitatu. (Kielelezo Na. 11)

Fedha za Mfuko wa Barabara zilizo-pelekwa TAMISEMI/TARURA kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wilaya zilikuwa shilingi milioni 167,365 kwa mwaka 2015/16 na kuongezeka hadi shilingi milioni 232,922 mwaka 2017/18. Jumla ya shilingi milioni 632,080 zilipelekwa TAMISEMI/TARURA kwa kipindi cha miaka mitatu (Kielelezo Na. 12)

Mgao wa Fedha za Mfuko wa barabara kwenda Wizara ya Ujenzi kwa ajili miradi ya maendeleo hususan kufanya upembuzi yakiniifu wa miradidi ya barabara ulikuwa jumla ya shilingi milioni 147,017. Mchanganuo wa umeoneshwa katika Kielelezo Na. 13

Baadhi ya Miradi Maalum Iliyogharamiwa na Fedha za Mfuko

Mbali na migao ya kawaida Bodi ya Mfuko wa Barabara imeweka kutoa fedha kwa ajili ya miradi maalum ya Barabara. Miradi hii imeweza kupunguza kero ya watumiaji barabara na kuongeza tija katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa kwa kutenga fedha maalum ni kama ifuatavyo:

- (i) Ujenzi wa mifereji ya maji katika eneo la Msasani Bonde la Mpunga: Mradi huu ulitekelezwa katika Manispaa ya Kinondoni na uligharimu shilingi 4,248,097,423.00 Mradi umesaidia kuondoa mafuriko ambayo hutokea kila mvua ikinyesha katika eneo la Msasani jijini Dar es Salaam na hivyo kuharibu mali na kuathiri afya za wakazi wa maeneo hayo.
- (ii) Matengenezo ya barabara ya Mwanza Airport: Mradi wa matengenezo ya barabara ya Pasians uligharimu kiasi cha shilingi 909,471,530.00. Matengenezo ya barabara hii yamepunguza msongomano wa magari na hivyo kuwezesha wakazi wa Mwanza wanaoishi katika maeneo yanayopitiwa na barabara hiyo pamoja na wasafiri wanaotumia Airport ya Mwanza kuweza kusafiri kirahisi.
- (iii) Ukarabati wa barabara za Hospitali ya Muhimbili: Matengenezo ya barabara za ndani ya Hospitali ya Taifa Muhimbili yaligharimu kiasi cha shilingi 1,125,820,300.00. Barabara zilizokuwa ndani ya hospitali ya Muhimbili zilikuwa katika hali mbaya sana. Ukarabati wa barabara hizo umeondoa kero ya muda mrefu kwa wagonjwa, wafanyakazi na wageni.
- (iv) Ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Mbande-Kongwa-Mpwapwa (km 5.0): Barabara hii ina urefu wa kilomita 50 na inaunganisha makao makuu ya mkoa wa Dodoma na makao



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John P. Magufuli akifungua barabara ya Bagamoyo Msata ambayo matengenezo yake yatagharamiwa na fedha za Mfuko.



Kivuko cha MV Kazi kinachofanya kazi kati ya Magogoni na Kigamboni kili-chonunuliwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara.

- (v) Ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Majimoto-Inyonga Town (km1.5): Mradi huu ulitekelezwa mkoani Katavi kwa kilomita 1.5 kama sehemu ya barabara inayounganisha makao makuu ya wilaya ya Mlele na Mpimbwe. Pia, utekelezaji wa mradi huu uligharimu jumla ya shilingi 1,200,000,000.00 na ulikamilika mwezi Juni, 2018.
- (vi) Ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Kandamija-Manda Bay (km 2.25): Barabara hii ni sehemu ya barabara ya mkoa ya Itoni -Ludewa-Manda yenye urefu wa kilomita 211 inayounganisha makao makuu ya mkoa wa Njombe na ziwa Nyasa. Mradi huu ulitekelezwa katika Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe kwa urefu wa kilomita 2.25 kwa gharama ya shilingi 3,042,854,650.00 na ulikamilika mwezi Juni 2016.
- (vii) Ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Mrunderunde-Mpeta (km 6.0): Mradi huu unatekelezwa mkoani Mtwara. Barabara hii ina urefu wa kilomita 69, na inaunganisha makao makuu ya wilaya ya Masasi na Newala. Utekelezaji wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa km 6 unaendelea na gharama yake ni shilingi 2,216,000,000.00.
- (viii) Ujenzi wa daraja la Furahisha: Ujenzi wa daraja

- (ix) Ununuzi na Matengenezo ya Vivuko: Fedha za Mfuko wa Barabara zimekuwa zikitumika kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipya, matengenezo ya vivuko pamoja na upanuzi na ujenzi wa maegesho ya vivuko. Katika mwaka wa fedha 2017/18 kiasi cha shilingi 2,036,625,634.00 zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipya kitakachokuwa kikifanya safari kati ya visiwa vya Kayenze na Bezi katika Ziwa Victoria. Aidha katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 hadi 2017/18 fedha zimekuwa zikitengwa kwa awamu na kuwezesha ununuzi wa vivuko vipya vya MV Kazi (Magogoni-Kigamboni), MV Tanga (Pangani - Bweni), MV Mwanza (Kigongo-Busisi).
- (x) Miradi ya kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam:
 - (a) Ujenzi wa Barabara ya Riverside- Makoka (km 1.8). Ujenzi wa barabara ya Riverside-Makoka wenye gharama ya jumla ya shilingi milioni 3,409 unagharimiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara na unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ilikamilika mwaka 2017 na awamu ya pili itakamilika mwaka huu wa fedha.

- (b) Barabara ya Tegeta Kibaboni - Wazo Hill - Goba - Mbezi Mwisho (km 20). Awamu ya kwanza kuanzia Goba mpaka Mbezi Mwisho (km 7), ujenzi ulianza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2016 kwa gharama ya shilingi 6,768,363,462.00. Awamu ya pili sehemu ya Goba-Madale (km 5), ujenzi wake ulianza Oktoba 2017 na unategemewa kukamilika Machi 2019.
- (c) Barabara ya Kilungule (Maji Chumvi) - External/Mandela (km 3.3). Ujenzi ulianza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2015 kwa gharama ya shilingi 4,448,783,969.00.
- (d) Barabara ya Kinyerezi-Kifuru-Malambamawili-Msigani-Mbezi (km 10.0) Awamu ya kwanza sehemu Kifuru- Kinyerezi (km 4), ujenzi ulianza mwaka 2014, na kukamilika mwaka 2016 kwa gharama ya shilingi 5,764,098,952.00 Awamu ya pili, sehemu ya Kifuru-Msigani (km 4), ujenzi ulianza Desemba 2016 na kukamilika Desemba 2017 kwa gharama ya shilingi 9,837,319,348.00.
- (e) Barabara ya Tabata Dampo - Kigogo Mwisho (km 1.6). Ujenzi ulianza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2016 kwa gharama ya shilingi 1,806,503,614.00
- (f) Barabara ya Ardhi - Makongo-Goba (km 9.0). Awamu ya kwanza, sehemu ya Goba-Makongo juu (km 4.0), ujenzi ulianza Februari 2017 na kukamilika Februari 2018 kwa gharama ya shilingi 15,354,828,724.18.

Miradi Mingine iliyotengewa fedha Katika Mwaka 2017/18 na 2018/19 ambayo utekelezaji wake uko katika hatua mbalimbali ni kama ifuatavyo:

- (i) Ujenzi wa barabara ya Kituo cha Afya Muriet- Arusha- shilingi 500,000,000.00
- (ii) Kufungua barabara ya Mawengi - Makonde Wilayani Ludewa-shilingi 500,000,000.00
- (iii) Ujenzi wa mitaro ya maji Tuan-goma block 5 na Masaki - Malela- Kigamboni Dar es Salaam shilingi 500,000,000.00
- (iv) Matengenezo ya barabara ya Minyenyi - Milongori - Wilayani Hanang - shilingi 500,000,000.00

- (v) Matengenezo ya barabara Kashura ya lami (km 1), Manispaa ya Bukoba - shilingi 500,000,000.00
- (vi) Matengenezo ya barabara ya Lupila - Kipengele, Wilayani Makete-shilingi 500,000,000.00
- (vii) Matengenezo ya barabara (km 1), Kibaha eneo la uwekezaji - shilingi 500,000,000.00
- (viii) Ujenzi wa barabara ya Kibo - Mamanku (km 1.1). Wilayani Korogwe- shilingi 800,000,000.00
- (ix) Ujenzi wa barabara ya Goba - Makongo pamoja na kulipa fidia- shilingi 1,179,454,259.00
- (x) Ujenzi wa daraja la Rungwizi katika barabara ya Saza-Kapalala mkoani Songwe- shilingi 1,162,905,340.00
- (xi) Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika wilaya ya Kilolo mkoani Iringa - shilingi 450,000,000.00
- (xii) Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma - shilingi 450,000,000.00
- (xiii) Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami barabara ya Boma na barabara za Tarime mjini katika wilaya ya Tarime mkoani Mara - shilingi 900,000,000.00

Mipango ya baadae

Bodi imeweka mikakati mbalimbali kwa ajili ya kuboresha maeneo ya mapato na matumizi ya fedha za Mfuko kwa Wakala wa Barabara katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama:

- (i) Kuongeza wigo na vyanzo vipya vya mapato ya Mfuko kwa kufanya tafiti ya vyanzo vipya na mabadala vya mapato ya Mfuko kutokana na mabadiliko ya teknolojia kwenye matumizi ya mafuta kwa vyombo vinavyotumia Barabara.
- (ii) Kusaidia kufanya tafiti mbalimbali za matengenezo ya Barabara kwa kutumia teknolojia mpya na nafuu ili kupata ubora wa kazi za barabara na kupunguza gharama za matengenezo ya barabara.

Wito kwa watumiaji barabara

Bodi ya Mfuko wa Barabara inatoa wito kwa wananchi na watumiaji wote wa barabara kuzitunza barabara ili ziweze kudumu kwa kutoharibu miundombinu ya barabara kwa kutoa vyuma kwenye madaraja na makalavati, kutongoa alama za barabarani, kutopitisha mifugo katika barabara hizo, kutovujisha mafuta na vilainishi kwenye barabara na kutozidisha uzito wa mizigo. Pia madereva wazingatie sheria na alama za barabara ili kuepuka ajali ambazo zinaleta uharibifu wa miundombinu ya barabara, mali na maisha ya watu. Uharibifu huu unarudisha nyuma juhudi za Serikali kuboresha miundombinu ya barabara.

Hitimisho

Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imetilia mkazo matengenezo ya barabara kwa wakati muafaka ili kulinda na kuzihifadhi barabara kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa kitaifa na kuongeza hali bora ya jamii. Huu ni uamuzi wa kimkakati kwa manufaa ya kizazi cha sasa na cha baadaye. Bodi itaendelea kuhakikisha kwamba barabara zetu zinapata matengenezo ya kutosha na kwa wakati ili ziweze kupitika muda wote kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu.